

FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI

# Kuwa na Mapenzi Mema kwa Kanisa na kwa Ulimwengu

*FMKD Mpango Mkakati 2019-2024*




1 Utangulizi 02

2 Sisi ni Nani 05

3 Maono na Maadili 08

4 Safari Yetu kama Jumuiya 11

5 Muktadha Wetu Kimataifa 13

6 Vipaumbele vyetu vya Kimkakati 17

6.1 Kusaidia Uwepo wa Makanisa na Ushuhuda Unaotikisa katika Dunia 19

6.2 Kukuza Hadhi ya Utu, Haki na Amani 23

7 Njia zetu za Kufanya Kazi 29

8 Ubia 30

9 Uhimilivu wa Kiasasi wenye Kuleta Matokeo Yanayofaa 31

FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI

*Tumekombolewa kwa neema ya Mungu, kuwa jumuiya ya Kikristo, tukiishi na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya ulimwengu wa haki, amani na uliopatanishwa.*

# 1
# UTANGULIZI

*Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu* (Gal 3:28)

"Kuwa na mapenzi mema kwa Kanisa na kwa Ulimwengu " ni kichwa cha mpango mkakati wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) 2019 -2024, uliopitishwa na Halmashauri Kuu ya FMKD mwezi wa Julai 2018. Mpango huu utaongoza kazi za jumuiya ya makanisa katika ushuhuda wake wa Injili ya Yesu Kristo katika ulimwengu wote. Mpango huu unaeleza kwa muhtasiri safari tunayojiandaa kuianza pamoja kama jumuiya ya makanisa 148 yaliyo katika nchi 99.


Kichwa hiki ni ukumbusho kuwa tuna shauku kuhusu uwepo na ushuhuda wa makanisa na kuhusu kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuleta haki, amani na upatanisho katika ulimwengu huu.

Mpango mkakati unajenga msingi wake katika mpango uliopita, ukiwianisha mwendelezo na ubunifu. Unaangalia ahadi za msingi za FMKD: kuwasaidia wakimbizi na wale wanaohamishwa makazi katika nchi zao wenyewe, kuimarisha umoja, kuikuza theologia, kuyaimarisha makanisa kwa ajili ya kazi ya misheni. Pia inajenga msingi wake katika matokeo ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili, ujumbe wake, mapatano, na katika matamko ya Mkutano yaliyotolewa kwa umma wa dunia. Mpango mkakati huu unakiri kwa dhati maono na maadili ya FMKD, ukitoa ufafanuzi wa muktadha wa dunia tunamoishi na kuweka bayana mambo ya msingi yanayoweza kutuleta karibu na maono na malengo yetu.

Utakapo soma neno"sisi" katika mpango mkakati huu wakati wote linarejea jumuiya ya makanisa. Mpango mkakati unatusaidia kuweka kwa ufasaha kusudi letu na mwelekeo wa pamoja na unaongoza lengo la tutakachokuwa tunafanya pamoja kama jumuiya ya makanisa yenye mwamko, katika kutetea hadhi ya utu wa mwanadamu, haki na amani.

Nauweka mpango mkakati huu mikono mwa makanisa 148 ambayo ni wanachama wa FMKD. Hizi ni ahadi zetu za pamoja. Ni matumaini na matarajio yangu kuwa makanisa wanachama watatumia mpango mkakati huu katika mazingira yao, yakidumu katika kiini cha ahadi za jumuiya ya makanisa, yakiutumia mpango mkakati katika mazingira yao na kuchangia katika kazi za kimataifa - ndivyo tunavyotaka kuwa na kufanya kazi kwa pamoja katika ulimwengu huu.

Mpango mkakati huu uwe hamasa kwa ajili ya kazi ya jumuiya ya makanisa katika kutuleta kwa karibu zaidi na katika kutimiza maono ya kuwa "tumekombolewa kwa neema ya Mungu, na kuwa jumuiya ndani ya Kristo, tukiishi na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuufikia ulimwengu wenye haki, amani na uliopatanishwa."



*Askofu Mkuu Dkt. Panti Filibus Musa, Raisi wa FMKD.*



*Kuwa shirika ndani ya kanisa ni karama. Tumeunganishwa katika kulitangaza Neno la Mungu na katika ushirika mimbarani na madhabahuni.*

# 2
# SISI NI NANI

*Ikiwa imeanzishwa mwaka 1947, sisi ni jumuiya ya kimataifa ya makanisa wanachama 148 yenye jumla ya watu milioni 75 katika nchi 99. Tunashiriki urithi wa pamoja wa Kilutheri, ukijengwa na mazingira tofauti ambamo tunapata uzoefu na kushuhudia neema ya Mungu ikomboayo. Katiba yetu inaweka kwa muhtasari misingi ya ahadi kama ifuatavyo:*

**Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani:**

linaendeleza ushuhuda wa pamoja wa Injili ya Yesu Kristo na kuyaimarisha makanisa wanachama katika kupeleka utume wa kufanya misheni na katika juhudi zao kuelekea umoja wa Kikristo ulimwenguni;

linaendeleza, ulimwenguni kote na miongoni mwa makanisa wanachama, kazi za diakonia, kupunguza uhitaji wa kibinadamu, kukuza amani na haki za binadamu, haki za kijamii na kiuchumi, utunzaji wa uumbaji wa Mungu, na usawa katika ugawanyaji wa rasilimali;

linaendeleza kwa njia ya tafiti za pamoja kujielewa lenyewe na kuyaelewa makanisa wanachama yanayounda jumuiya na kuyasaidia makanisa kutenda kwa pamoja katika majukumu yao.

*Kutoka Katiba ya FMKD*

*Kujihusisha kwetu namambo ya dunia hii kunatokana na tendo la Utatu wa Mungu anayetuita, anageuza, na kutuzatiti ili kushiriki katika misheni Mungu ya kuleta haki, amani na upatanisho.*

Tunaielewa misheni ya Mungu kuwa ni kamili, inayohusisha kutangaza Injili, huduma ya diakonia (kumhudumia jirani na mazingira), kutetea hadhi ya utu wa mwanadamu, haki na amani.

Tunayaeleza mahusiano yetu kwa kutumia dhana ya kitheologia ya "jumuiya." Ni mwitikio kwa wito wa Mungu unaoyaleta makanisa pamoja.

- Kuwa pamoja kama makanisa katika jumuiya ni zawadi. Tumeungana katika kutangaza Neno la Mungu katika mimbara na katika ushirika madhabahuni. Tunaitwa kukusanyika pamoja katika imani ya Utatu wa Mungu, kushirikishana Neno na sakramenti ya Ubatizo na Ushirika Mtakatifu. Kwa pamoja tunasikia na kushirikishana habari njema za maisha ya Yesu, kifo, na ufufuo kama zinavyoshuhudiwa kwa njia ya Maandiko Matakatifu na kuelezwa katika Kiri za Kiekumene na Maungamo ya Kilutheri (Ungamo la Ausburg na Ketekisimo Ndogo).
- Kuwa makanisa katika jumuiya ni kazi na wajibu pia. Tunaposhirikishana zawadi ya kujumuika pamoja, tunasogezwa kwenye safari ya kiroho, inayotualika kusikilizana, kushirikishana furaha na mateso, kukua katika kuhudumiana, na kuzama katika kuelewa jinsi tunavyohitajiana kama washirika wa Mwili wa Kristo. Tunahitaji kushiriki katika kutoa mawazo yenye kuujenga ulimwengu, kwa kufuata misingi ya utambulisho wetu wa kitheologia na kwa ajili ya kuwa na imani ya pamoja katika Injili. Tupo tayari kufanya kazi katika mahusiano ya kiekumene na imani za dini nyingine, na pia kufanya kazi na asasi za serikali na zisizo za kiserikali.

Tunaahidi kuwa na umoja wa Kikristo, unaojengwa katika uelewa wa kuwa sisi ni sehemu ya Mwili wa Kristo. Hali hii inatokea kwa njia ya mazungumzo ya kitheologia na katika hudumu za pamoja na washirika wa kiekumene.

Sisi tunatambulika kimataifa kama asasi ya kidini inayotenda, inayoieleza imani kwa njia ya utetezi, kazi za kimaendeleo, na kujihusisha na kazi za kutoa misaada ya kibinadamu. Tuna ushirika na Umoja wa Mataifa (UM), kwa njia ya mawakala wake wengi. Tunatambuliwa rasmi na Baraza la Umoja wa Mataifa la Mambo ya Uchumi na Kijamii (UN ECOSOC).

Mungu anatuita kushuhudia kinabii, kuthibitisha hali ya kuwa tofauti, kuishi na tofauti, kuheshimu hadhi ya utu wa mtu, na kumhudumia jirani anayeteseka. Hivyo, kwa kufuata misingi ya mafundisho yetu, njia ya kuifikia dunia ni ile ya kuweka matumaini.



*Tunaielewa misheni ya Mungu kuwa ni mkabala wa jumla wa kutangaza Injili, kazi za huduma (kwa jirani) na utetezi wa utu wa mwanadamu, haki na amani.*

# 3
# MAONO NA MAADILI

Tunaueleza uelewa na wito wetu katika ulimwengu huu na kauli yenye maono haya:

*Tumekombolewa kwa neema ya Mungu, kuwa jumuiya ya Kikristo, tukiishi na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya ulimwengu wa haki, amani na uliopatanishwa.*

Maadili yetu yanatokana na imani. Yanajulishwa na masomo ya Biblia ambayo ni kiini cha mafundisho ya makanisa ya Kilutheri na yameendelea kuujenga utambulisho wetu kitheologia.

## Hadhi ya Utu na Haki

*Lakini hukumu na itelemke kama maji, na haki kama maji makuu (Amo 5:24).*

Kila mmoja na kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu, amepewa talanta na uwezo, na ana hadhi ya utu, bila kujali hali yake ya kijamii, jinsia, kabila, umri, uwezo, au tofauti zingine. Ahadi yetu ya kutetea haki za binadamu na haki [zingine] maana yake tunaanza kuyafanyia kazi yale mambo yanayosababisha umaskini na kutengwa kwa watu, na kupigania usawa wa mgawanyo wa madaraka, rasilimali na fursa.

## Huruma na Ahadi

*Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; alipomwona alimhurumia (Lk 10:33).*

Tukiwa tumehamasishwa na upendo wa Mungu kwa wanadamu, tunawiwa huruma ya kusimama na kuwatunza watu wanaoteseka - maskini, watu wanaoishi katika mazingira hatarishi na watu wanaofikiriwa kuwa ni wa hali ya chini na makundi ya watu wachache na wenye imani wanaopata shida ya ubaguzi, kutendewa vitendo vya ukatili, na wenye hali ngumu ya maisha katika mazingira mbalimbali ya ulimwengu huu.

## Kuheshimu Tofauti

*Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja, vivyo hivyo na Kristo (1Kor 12:12).*

Tofauti miongoni mwetu zinaeleza utajiri wa uumbaji wa Mungu. Kama ushirika wa kimataifa wa makanisa, tunathamini na kutafuta kuelewa tofauti zetu kitamaduni, kihistoria, na kimazingira, na jinsi tofauti hizi zilivyojenga uelewa wetu wa kitheologia, na mitazamo yetu dhidi ya masuala ya kimaadili na mifumo yake, na ushiriki wetu katika misheni ya Mungu.

## Kujumuisha na Ushiriki

*"Basi enendeni hata njia panda za barabara, na wote mwaonao waiteni arusini" (Mt 22:9).*

Tunaahidi kujumuisha na kuwezesha ushiriki kamili na wenye usawa wa wanawake, wanaume na watu wa marika yote na makundi ya makabila mbalimbali, pamoja na watu wenye ulemavu, katika maisha ya kanisa na jamii na katika michakato mbalimbali ya maamuzi, na shughuli na programu za FMKD. Tunaelewa kuwa mienendo ya nguvu [za kisiasa, kiuchumi na kijamii], kanuni za tamaduni, uwezo wa kutumia rasilimani, na sababu zingine vimeleta vikwazo vya ushiriki na tunafanya kila njia kuviondoa.

## Uwazi na Uwajibikaji

*"...'Amini, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi' " (Mt 25:40).*

Tunawajibu kama mawakili wa rasilimali na majukumu ambayo Mungu amekasimu kwetu. Tunaahidi kuwa wazi katika malengo yetu, michakato, na maamuzi, na kutumia rasilimali na kuwajibika kwa watu tunaowahudumia, makanisa wanachama, wenye udugu na sisi, na wafadhili.



*Mchakato huu unaothibitisha maana ya kuwa ushirika wa kikanisa kwa mtazamo wa Kilutheri, na jinsi ushirika unavyoishi si kwa ajili yake tu bali kwa kuhudumia na kutoa ushuhuda wake katika ulimwengu wote.*

# 4
# SAFARI YETU KAMA JUMUIYA

*Katika miaka ya karibuni, safari yetu na ushuhuda vimehabarishwa kwa njia ya kusherehekea miaka 500 ya kumbukumbu ya Matengenezo chini ya mada "Tumekombolewa kwa Neema ya Mungu" na mada tatu ndogo "Wokovu - si wa kuuza," "Binadamu - si wa kuuza," na "Uumbaji - si wa kuuza." Mada hizi zimeboresha kwa kiasi kikubwa na ushiriki wetu kwa njia ya kuwa na mpango.*

Kumbukumbu ya Matengezo ilikuwa kichocheo kwa maendeleo ya kiekumene, huku kukiwa na mafanikio kadhaa, kama vile sherehe ya kumbukumbu ya pamoja Matengenezo kati ya Wakatoliki na Walutheri kule Lundi, Swedeni, na kupanua uwigo wa Tamko la Pamoja la Mafundisho ya Kuhesabiwa Haki, kutoka kuwa tamko la makanisa mawili hadi kuwa la makanisa mengi.Ilitoa nafasi ya kuwa na ushiriki wa pamoja katika kutafsiri maandiko na kujihusisha kufikiri kwa pamoja juu ya nafasi ya theologia na kanisa katika jamii. Kumbukumbu ya Matengenezo ilitoa hali ya umoja ulioruhusu kutoa ushuhuda pamoja, wakati huo huo tukishughulikia tofauti zilizo ndani ya jumuiya.

Tumejihusisha na mchakato wa kujitambua kama jumuiya ya Kilutheri. Mchakato huu umethibitisha nini maana ya kuwa na jumuiya ya kikanisa kwa mtazamo wa Kilutheri na jinsi jumuiya inavyoishi, si yenyewe tu bali katika kuhudumia na kushuhudia katika dunia.

Tumeendelea kukua pamoja kama jumuiya ya makanisa tukiongeza hali ya kuchangamana na kushirikiana katika ngazi ya kanda na kimataifa.

*Tuliweka mkazo katika kuunganisha maeneo mbalimbali na tulidumu pamoja hata pale tulipopata changamoto ya kuwa na tofauti miongoni mwetu.*

Katika hali ya wimbi kubwa la ukimbizi na hali ya watu kulazimishwa kuyahama makazi yao, bado tulikuwa na uwezo wa kuonyesha utayari wetu, na kwa sasa tumewafikia kiasi cha watu milioni tatu. Katika kufanya hivyo, tumepanua uwingo wa washirika wetu, tukijumuisha washirika wapya wa madhehebu mengine na washiriki toka dini zingine.

Tumeimarisha kazi yetu na vijana, ambao walituongoza katika uimarishaji wa kujitolea kwetu katika kutatua tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na wametusadia kuelewa kuwa hili ni jambo la haki kati ya kizazi na kizazi kingine.

Tumepitisha Sera ya Haki ya Jinsia ambayo iliweka msingi wa utekelezaji katika mazingira ndani ya makanisa wanachama.

Katika Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili (Windhoek, Namibia, 2017) makanisa wanachama wa FMKD yalikuja pamoja na kuthibitisha safari yao ya pamoja. Ujumbe wa Mkutano, mapatano, na matamko kwa umma yanatoa nafasi ya kufikiri pamoja kama jumuiya ya makanisa ya kimataifa kuhusu safari hii. Wanakubali kuwa mada zifuatazo ni za muhimu kwa ajili ya ushuhuda wa pamoja katika ulimwengu: kuijenga jumuiya, makanisa na wajibu wao kwa kazi za misheni, elimu ya theologia, ahadi za kiekumene, uhusiano na dini zingine, utetezi, haki ya kimazingira, utambulisho wa Kilutheri, ushiriki wa vijana na wanawake katika uongozi, haki ya jinsia, utoaji misaada kwa watu waliokumbwa na majanga, kazi za maendeleo, kuwasaidia wakimbizi na watu waliohamishwa kwa nguvu, na wahamiaji.

# 5
# MUKTADHA WETU KIMATAIFA

*Safari yetu kama ushirika wa makanisa inachukua nafasi ndani ya anga za kimataifa zinazobadilika kila wakati. Hapo chini kuna baadhi ya mambo yanayosababisha mabadiliko katika dunia ya leo. Kutambua na kuchambua viashiria hivi vya mabadiliko kunatuaarifu uhusika wetu kama ushirika wa makanisa.*

**Kimataifa, nje**

- Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika kupunguza umaskini, viwango vya kutokuwa na usawa kitaifa na kimataifa bado kinazidi kukua.
- Kuna mantiki ya soko lililopo ambalo linachukua nafasi ya kwanza na kuhubiriwa katika jamii juu ya mambo ya kijamii na kimazingira.
- Matokeo imara ya mfumo wa haki za binadamu yameanza kusongwa zaidi. Kuna hali inayokuwa ya kujaribu kuvunja haki za binadamu, haki za kimataifa za misaada ya kibinadamu, na uhuru wa kidini. Haki za watoto, wanawake, na makundi ya watu wanaotunza asili zinakandamizwa.
- Kukua kwa ukatili na kuongezeka kwa migogoro na kukosekana kwa utengemano kumeongeza watu kuyahama makazi, wakimbizi, na wahamiaji.
- Kuna kukua hali ya kutukuza utaifa, hifadhi ya misingi ya dini, chuki kwa wageni, siasa kali, ubaguzi wa rangi, mifumo ya serikali/siasa inayojali maoni na fikra za watu, mifumo ambayo inayotumia uwoga wa watu kupata uhalali na kueneza hali ya wasiwasi.

- **Mabadiliko ya tabia nchi yanaendelea**, na watu wanaoishi katika mazingira hatarishi wakichukua mzigo mzito.

- **Nafasi ya Asasi zisizo za kiserikali** inazidi kupungua katika jamii, na uhalali na maana ya watendaji wa asasi hizo ukizidi kujadiliwa, kukua kwa hali ya serikali kuthibiti [watu] kitaifa, na kukua kwa ushawishi wa sekta binafsi.

- **Kupungua kwa ahadi za misaada** kunaathiri misaada ya kibinadamu na kazi za maendeleo.

- **Mafundisho ya kidini na majimbo** yanatumika kwa sababu za kisiasa.

- **Mifumo ya Kidijitali** inabadilisha jinsi watu wanavyowasiliana na kuhusiana wenyewe kwa wenyewe, mashirika yanavyofanya kazi, ubadilishanaji wa taarifa, upashanaji habari, na namna ya kuathiri maoni ya umma, utengenezaji wa sera, na jinsi inavyobadilisha jamii kwa ujumla.

- **Mifumo mipya ya kimataifa** imeundwa, ambayo inajaribu kutatua baadhi ya mambo haya yaliyobayana: Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (MME), Agenda ya Makubaliano Makubwa na Uenyejizaji, Makubaliano ya Hali ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi, Maafikiano ya Kimataifa juu ya Wakimbizi.

- **Mashirika ya Kidini yameendelea kutambuliwa hasa na**Umoja wa Mataifa kuwa washirika hai katika kujenga jamii himilivu na katika kupigania haki na amani; na wakati huo huo, kuna hali ya kuzibagua kanda kutoka kwenye anga za umma wa kimataifa.

- Kuongezeka hali ya **kutambua thamani ya mjadala wa kidini** na mahusiano na namna inavyochangia katika kuleta amani.

- **Mabadiliko ya Ukristo kimataifa:** makanisa Kusini mwa Dunia yanakua na Kaskazini mwa Dunia yanapungua; mabadiliko haya yanaonekana pia katika maisha ya FMKD.

- **Mabadili ya nchi kidini:** makanisa ya kivipaji na kiinjili na namna mpya za ibada za kiroho vimeshika

kasi; jamii zinaanza kuwa na tofauti kubwa kidini.

- **Kukutana** kati ya familia za dini mbalimbali **kumekuwa** kukiashiria matokeo ya kihistoria yaliyofikiwa katika mijadala ya pamoja, wakati huo huo **mipasuko mipya kuhusu mambo ya kimaadili** ikijitokeza miongoni na ndani ya makanisa, wakati mwingine ikipanga upya mahusiano ya kimadhehebu na kidini.
- **Uhasama umeongezeka** kati ya jumuiya za kidini, na mara nyingi ukifungamanishwa na utambulisho wa kisiasa, na kuwa na madhara makubwa kwa jumuiya za kidini zinazoishi kama kundi la watu wachache.
- **Watendaji wapya wa kidini** wanashawishi mazungumzo na maamuzi ya kisera katika anga la umma.

**Maendeleo haya na viashiria hivi vinaathiri kanisa kimataifa, na kushawishi FMKD na makanisa washirika kuwa kama sehemu ya Mwili wa Kristo.**



*Tunaishi na kufanya kazi pamoja, pale tunapoendelea kuitikia wito wa Mungu na kushiriki katika misheni ya Mungu katika ulimwengu wote.*

# 6
# VIPAUMBELE VYETU VYA KIMKAKATI

*Kufanyika tao juu ya msingi wetu wa kuendelea na ushuhuda, umewekwa kwa wito kwenda kwa wanachama wa makanisa ya FMKD kuishi na kufanya kazi pamoja kama ushirika wa makanisa katika haja inayoendelea ya matengenezo.*

Wito huu, umejengewa msingi katika ibada na sala, vyote ni msingi wa ushuhuda wa pamoja katika dunia na ukweli kwamba tunaendelea kukua ndani yake. Ni wito ulio na umhimu wa ndani kiroho na kitheologia. Unahusisha msingi na muktadha ambapo katika hayo tunatenda ndani ya dunia hii.


Kwa kujenga juu ya safari yetu inayoendelea na matokeo ya Mkutano Mkuu na katika mazingira tunamoishi, tunatambua vipaumbele viwili vya kimkakati kwa kipindi kilicho mbele yetu:

- Kuunga mkono uwepo wa makanisa na ushuhuda unaoitikisa dunia.
- Kukuza hadhi ya utu, haki na amani.

Mfumo huu na vipaumbele viwili vya kimkakati vinavyotokana nao vinaweza kuelezwa katika umbo kama ifuatavyo.

Katika kiini cha kazi yetu ni wito wetu wa kuishi na kufanya kazi pamoja kama ushirika wa makanisa katika kuendeleza matengenezo. Huu si ukweli uliodumaa, na sio wenye mwisho wake wenyewe: Tunaishi na kufanya kazi pamoja, tunapoendelea kuitikia wito wa Mungu na tunaposhiriki katika misheni ya Mungu ndani ya dunia. Kwa kufanya hivyo, tunalenga kusaidiana kushuhudia kwa kishindo ndani ya mazingira yetu yaliyotofautiana na kukuza hadhi ya utu, haki na amani. Mistari katika mchoro hapo juu inayotenga mihimili hii imetawanyika kuonyesha mwiingiliano kati ya vipaumbele vya kimkakati na mahusiano yake na kiini cha ukweli wa kuwa makanisa shirika.

**Maelezo kuhusu mpango mkakati, vipaumbele na misingi yake**



## 6.1 Kusaidia Uwepo wa Makanisa na Ushuhuda Unaoitikisa Dunia

*Tunashauku juu ya makanisa yanavyomshuhudia Kristo kikamilifu katika mazingira yao. Tunatafuta kujizatiti na kuwekeana rasilimali miongoni mwetu ili kuishuhudia neema ya Mungu ikomboayo. Changamoto ambazo makanisa yanakumbana nazo zinatofautiana kwa asili, kutokana na mazingira yao. Kwa kujihusisha na mazungumzo na mahusiano, tunaimarishana na kutunzana.*

### Kama ushirika wa makanisa, tunaendelea kufanya kazi pamoja:

**Kukuza kwa pamoja mjadala wa kitheologia unaotafuta kueleza kwa ufasaha uelewa wetu kuhusu kuwa makanisa ya Kilutheri ndani ya ushirika**

- Tutaendelea kukuza uelewa wa pamoja wa utambulisho wa kitheologia wa makanisa wanachama ya FMKD ambao utayawezesha kuendelea kutambuana, kuwa ni sehemu ya ushirika, wakati yakishuhudia katika mazingira yao tofauti.
- Tunashirikiana kufanya kazi pamoja kutambua na kutatua masuala ambayo yanawakilisha changamoto za kitheologia kwa makanisa yetu leo.
- Tutakuza msingi wa kitheologia na masimulizi ili kuimarisha uhusika wa makanisa na ushirika na uhusika wa ushirika katika anga za umma.

**Kuyaishi mahusiano ya kiushirika kati ya makanisa wanachama**

- Tutaendelea kubaini na kueleza wazi kabisa uelewa wetu wa pamoja, mifumo, na desturi zinazosaidia makanisa yanapoelezea wito wao wa kuishi ndani ya ushirika.
- Tutatoa ushirikiano na kuunga mkono mapambano na utambuzi wa kitheologia na kuelewa na kutatua tofauti na migogoro ndani ya ushirika wetu.

**Kufanya kazi pamoja kueendeleza misheni kamili ya Mungu**

- Tutasaidia uwezeshaji wa makanisa wanachama kwa ajili ya kuhubiri, kuhudumu, na kazi za utetezi.
- Tutaendeleza michakato na mifumo kuwezesha elimu ya kitheologia na uumbaji.
- Tutatatua changamoto na kuangalia fursa zinazotokana na kukua na kupungua kwa wanachama katika kanisa.
- Tutahamasisha maendeleo ya uwajibikaji wa walei na uongozi wa wachungaji katika kanisa.

**Kukuza utetezi wa haki kijinsia katika nyanja zote za kijamii**

- Tutasaidia kutekelezwa kwa Sera ya Haki ya Jinsia katika makanisa wanachama.
- Tutafanya kazi kuendeleza mahusiano yenye kujali haki kati ya wanawake na wanaume, na yanayotoa mwanya wa mazungumzo kuhusiana na majukumu ya kijinsia na elimu kuhusu mifumo ya kiume.
- Tutakuza uongozi wa wanawake ndani ya kanisa na jamii na ushiriki wa kijinsia wenye usawa katika mijadala na michakato ya maamuzi.
- Tutakuza kushirikishwa kwa wanawake katika huduma ya kichungaji.
- Tutahakikisha na kuendeleza nafasi na mifumo ya ushiriki wenye haki kijinsia katika maisha ya ushirika wa kimataifa.



*Tutasaidia kuyajengea uwezo makanisa wanachama kutangaza, kuhudumu na kufanya utetezi*

**Kuhakikisha ushiriki wenye maana wa vijana katika kanisa na jamii**

- Tutahakikisha tunaweka nafasi na mifumo kwa ajili ya kuendeleza ushiriki wa vijana katika maisha ya ushirika wa kimataifa.
- Tuhamasisha uhusika wa kimarika katika masuala yenye manufaa kwa ajili ya kanisa na jamii.
- Tutasaidiana kuhakikisha ushiriki wa vijana katika michakato ya maamuzi ndani ya makanisa wanachama.

**Kuwahusisha washirika na kujenga mahusiano ili kuitikia wito wa kuwa na umoja na ushuhuda wa pamoja**

- Tutasonga mbele na ahadi yetu ya kutafuta umoja wa Mwili wa Kristo kwa kushirikiana na washirika wetu wote wa madhehebu mengine.
- Pamoja na washirika wa madhehebu mengine, tutaimarisha kuingiliana katika michakato ya mafunzo ya kitheologia, kushirikiana katika sala, na kuja pamoja kwa huduma za kidiakonia.
- Tutadumisha uwajibikaji wa kichungaji katika mijadala yetu ya kitheologia na kutafuta majibu ya changamoto za kiekumene katika jumuiya za makanisa wanachama pale yalipo.

**Kujihusisha na mazungumzo na dini zingine na uhusiano ili kujenga uelewano na kukuza ushirikiano.**

- Tutachangia mitazamo ya kitheologia ya Kilutheri katika mazungumzo yetu na dini zingine.
- Tutaendelea kujifunza kutoka dini zingine na kukuza elimu ya dini zingine miongoni mwa jumuiya na viongozi wa dini.
- Tutayazatiti makanisa wanachama ili yajenge mahusiano na dini zingine katika mazingira yao.
- Tutasaidia mipango ya madhehebu katika utetezi na diakonia, ili kuleta matokeo chanya na kujenga madaraja kati ya jumuiya zinazoamini [dini zao].

## 6.2 Kukuza Hadhi ya Utu, Haki na Amani

*Kwa kusukumwa na imani na tafsiri za kitheologia, tunaahidi kudumisha hadhi ya utu na kazi kwa ajili haki na amani. Hii inajumuisha kudumisha hadhi ya uumbaji na kudumisha haki za binadamu kwa kila mtu. Kwa kujenga katika ushuhuda wa makanisa wanachama wa FMKD pale yalipo, tunanuia kuzieleza ahadi hizi kama ushirika wa makanisa wa kimataifa. Katika kufanya hivyo tunatafuta kuyapatia majibu mateso ya watu na kuondoa mizizi ya sababu zake.*

### Kama ushirika wa makanisa, tutafanya kazi pamoja:

**Kutoa majibu kwa watu wanaokumbwa na majanga, tukilenga kuwasaidia wakimbizi, wanaoyarudia makazi yao, watu waliohamishwa kwenye makazi yao, wenyeji wa wakimbizi, na jumuiya zilizo katika hatari**

- Tutaendesha oparesheni kama ushirika wa kimataifa tukihimiza haki na ulinzi, uwezo wa kuchuma riziki na kupata huduma.
- Tutafanya kazi kwa njia ya kufungamanishwa na kukamilishana katika ngazi ya mtu, jumuiya, na taasisi.
- Tutaunganisha misaada ya dharura na kazi za kuwapa waliopatwa na majanga nafuu na kazi zitakazosaidia kuwaletea maendeleo ya muda mrefu.

**Kusaidia jumuiya mahali zilipo katika juhudi zao za kutafuta maendeleo endelevu ili watu wake wapate maisha yenye hadhi na na yenye kuwafanya wafurahie kikamilifu haki zao**

- Tunalenga watu wanaoishi katika mazingira hatarishi na wanaotengwa, na kuhimiza njia yenye kujali haki katika hatua zetu zote tunazochukua.
- Tutabadilika haraka kwa kufuata muktadha unaobadilika ili kuhakikisha uhimilivu wa kijamii na kimazingira.
- Tutahakikisha kazi yetu inaendana na misingi ya makusudio ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makubaliano Makubwa.



*Tutayahimiza na kuyawezesha makanisa wanachama kushiriki kikamilifu kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu.*

**Kuyazatiti makanisa wanachama ili kujihusisha na kazi za diakonia**

- Tutayajengea uwezo makanisa wanachama ili yaweze kutatua changamoto kwa uhimilivu katika maeneo yao kwa njia ya huduma ya diakonia.
- Tutayasaidia makanisa kushughulikia mahitaji ya kidiakonia kwa njia ya miradi maalumu.
- Tutayahimiza na kuyazatiti makanisa wanachama kujihusisha na Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kuleta matokeo yanayofaa.

**Kushirikiana na washirika wa madhehebu mengine, watendaji wa dini zingine, na viongozi wa dini katika masuala yahusuyo hadhi ya utu, haki na amani**

- Tutafanya kazi pamoja, pale inapobidi, ili kuchangia kazi za pamoja, kuziwajibisha serikali na kukusanya nguvu ya watu ili kudumisha hadhi ya utu na kutetea uhai/uzima wa mazingira.
- Tutaendeleza ahadi yetu katika nyanja zote na kupanua ushirikiano ili kuunga mkono kwa pamoja maendeleo endelevu.

**Kuimarisha juhudi kwa ajili ya haki ya mazingira**

- Tutaunga mkono juhudi za makanisa katika kuyaelimisha juu ya mabadiliko ya tabia nchi na hatua yanazotakiwa kuzichukua.
- Tutachangia moja kwa moja katika juhudi za kupunguza makali ya tabia nchi na kuyawezesha makundi yanayoishi katika mazingira hatarishi kukabiliana na hali hiyo.
- Tutaimarisha utetezi ili kuzuia mabadiliko ya tabia nchi katika ngazi zote za jamii.

**Kuimarisha utetezi katika ngazi za kimaeneo na kimataifa ili kukuza haki za binadamu na kulinda haki za jumuiya za makundi yanayotengwa**

- Tutajenga katika uzoevu na elimu toka ngazi za chini ili kuleta masuala ya haki za binadamu kutoka chini kuja kwenye uwanja wa kimataifa.
- Tutakuwa mstari wa mbele kupambana katika masuala ya haki, na katika kuleta usawa wa kiuchumi.
- Tutayatia moyo makanisa wanachama na programu katika nchi zao kutetea [haki za binadamu] na kujenga muungano na watendaji wa mashirika ya dini na makundi ya asasi mbalimbali katika maeneo yao.
- Tutayahimiza mataifa washirika wa UM kudumu katika kanuni, vyombo, na makubaliano ili kuokoa hadhi ya utu na uzima wa uumbaji wa Mungu.




*Tutajenga katika uzoefu na ufahamu unaotokana na watu wa chini ili kuleta mambo na ukweli wa haki za binadamu za wenyeji kwenye uwanja wa kimataifa.*

# 7
# NJIA ZETU ZA KUFANYA KAZI

*Katika kazi zote, tunajitahidi kuwa wabunifu na waanzishaji, tukitumia njia ambazo ni elimumwendo na tukiwekea maanani mada, muktadha, mahitaji, ufanisi na uwajibikaji.*

Mkutano Mkuu wa FMKD na Halmashauri Kuu, kama vielelezo vya ushirika, vinatoa mwelekeo wa kazi yetu. Ofisi ya FMKD inatenda kwa niaba ya fungamano, ikiandamana na makanisa wanachama katika maeneo yao na kuratibisha na kutekeleza majukumu ya pamoja. Katika kufanya kazi yake, ofisi ya fungamano inatumia mbinu na njia zifuatazo.

**Mawazo na utambuzi wa kitheologia**

- Kuleta pamoja mitazamo ya kitheologia kwa ajili ya kukuza mawazo ya kimaeneo na mwingiliano wa kimaeneo na kitamaduni kwenye ngazi ya kimataifa.
- Kujifunza toka kwa kila mmoja katika roho ya kukuza upendano.
- Kulea elimu ya kitheologia
- Kukuza mwingiliano wa kifani na kazi ya kitheologia katika ngazi ya kitaaluma.

**Kuandamana na makanisa wanachama**

- Kutembea pamoja kwa upendano na mshikamano, na kusadiana ili kushiriki katika misheni kamili ya Mungu
- Kutembea pamoja kama vielelezo vya kimaeneo vya ushirika
- Kujihusisha katika muungano wa hiari na mitandao kwa ajili ya kufanyia kazi mada mbalimbali
- Kuwa na mshikamano kati yetu wakati wa kukumbwa na changamoto na kutafuta namna ya kuzitatua
- Kuwasiliana juu ya maisha na kazi za makanisa wanachama na ushirika ili kuimarisha kujitambua, ufahamu, na mahusiano

**Kuitisha na uwezeshaji**

- Kuyakusanya makanisa na asasi ili kuyafanyia kazi masuala yanayokabiliana nayo katika maeneo na kama sehemu ya ushirika wa kimataifa
- Kuendeleza ufahamu na matendo mema kwa njia ya mafunzo ya pamoja na kuingiliana

**Kutekeleza moja kwa moja**

- Kuwa na operesheni katika kazi za misaada na maendeleo, kuitikia katika utoaji wa misaada ya dharura, na kung'oa mizizi ya sababu za mateso na uonevu
- Kujihusisha kimataifa na ushirikiano wa kimadhehebu
- Kutoa matamko katika ngazi ya umma wa kimataifa

**Utetezi**

- Kutetea kwa njia na kuwa pamoja na makanisa wanachama na programu za nchi husika na kusaidia kazi za utetezi katika maeneo yao
- Kutetea wajibu wa makanisa kama sehemu ya asasi za jamii katika anga za umma.
- Kutetea uhuru wa dini, haki jinsia, haki za wakimbizi na haki ya mazingira

**Kuunganisha maeneo na jumuiya ya kimataifa**

- Kuleta pamoja sauti kutoka kanda na makanisa wanachama ili kuweka mizizi ya kazi za kimataifa katika hali halisi ya mahitaji ya kimaeneo
- Kupaza sauti katika ngazi ya kimataifa, ili kuziwajibisha serikali za kitaifa katika ahadi zake za kimataifa
- Kuleta uzoefu wa jumuiya za kimaeneo ili kushawishi maamuzi ya kisera kimataifa na kusimamia utekelezaji wake

**Kufanya kazi na wengine**

- Kufanya kazi na washirika kwa ajili ya kukuza thamani upendano na kuunganisha nguvu ili kufikia malengo ya pamoja.

# 8
# UBIA

*Mahusiano ya kimkakati ni muhimu kwetu. Yanachukua sura nyingi nakuhudumia makusudio tofauti ndani na nje ya ushirika. Tunahusika kimkakati na wabia wetu kubadilishana ufahamu na kushirikiana katika kutumia rasilimali, ili kuhusiana, kuchukua hatua, na kuimarisha uratibishaji, na kupanga na kutekeleza programu kwa pamoja.*

Tunatambua ubia ufuatao kama msingi katika miaka ijayo:

- ubia na makanisa wanachama na taasisi zake, pamoja na taasisi za kitheologia na mitandao yake
- wabia wa madhehebu mengine na dini zingine
- ubia na jumuiya yalipo makanisa, asasi za kijamii, asasi za maendeleo na misaada ya kibinadamu, na watendaji wa serikali
- mfumo wa UM na mawakala wake maalumu

# 9
# UHIMILIVU WA KIASASI WENYE KULETA MATOKEO YANAYOFAA

*Ili kufikia malengo ya mpango huu wa kimkakati na kuwa asasi himilivu na zenye kuleta matokeo chanya, tutaendelea kuwekeza katika maendeleo ya kiasasi katika maeneo yafuatayo.*

## Uongozi wa kimkakati katika ngazi zote

Uongozi katika FMKD unachukua nafasi katika ngazi tofauti. Uongozi unaakisi utajiri mwingi wa ushirika, unadumisha usawa wa kijinsia, na kuhakikisha kuwa na uwakilishi wa vijana.

Halmashauri Kuu na ofisi ya fungamano vinahitaji kuzatitiwa vizuri na kusaidiwa ili kuviwezesha kuiongoza asasi katika kutekeleza mpango mkakati. Kwa kusudi hilo, tutafafanua na kutia makali uelewa wa majukumu na nyajibu za uongozi wa Halmashauri Kuu na ofisi ya fungamano.

## Utawala kamambe wa fedha na ukusanyaji rasilimali

Katika mabadiliko ya kiuchumi kijiografia, tutaitikia kupata fursa mpya za kifedha na kujibu changamoto zake. Hii inahitaji kuimarisha uwezo na taaluma ya watumishi. Ushirikiano thabiti wa ndani katika kukuza rasilimali ni muhimu kwa ajili ya uhimilivu wa kifedha wa FMKD.

Kama mawakili na wawajibikaji, tutaendelea kukuza na kuimarisha utawala wa kifedha. Ofisi ya fungamano inaahidi kuweka michakato ya uwazi na itatoa ripoti sahihi na kwa wakati. Kuweka taratibu zinazofaa za kutoa ripoti zitasaidia kujenga imani kubwa ya wafadhili watoaji misaada wa sasa na wapya.

## Kupanga miundo na mifumo

Tunapenda kuongeza ufanisi na ubora katika miundo na michakato yetu. Tutahakikisha uwazi katika kazi za kimipango za ofisi ya fungamano.

Tunataka kuwekeza katika mifumo ambayo ni ya manufaa kwa gharama nafuu na kusadia FMKD katika kuwa la kimataifa, asasi ya kimtandao, kuwa na uwezo wa kupata taarifa, mawasiliano ya wakati, na mahusiano yaliyounganishwa kimtandao. Miundombinu ya kidijitali na eneo linalomilikiwa sehemu mbili litawezesha kuifikia mifumo na miundo.

## Kuwekeza katika rasilimali watu

Tutatengeneza njia mkakati kwa ajili ya watumishi wetu ili kudumisha nguvu kazi yenye ushindani wa hali ya juu. Hii inajumuisha uwekezaji katika kuajiri, kuendeleza watumishi, na uongozi katika mbinu za utawala. Tutaboresha mifumo ya rasilimali watu na kuwasaidia watumishi kutekeleza majukumu yao. Tutalenga katika kuboresha hali za watumishi na kuimarisha kinga na usalama wao.Tutalea utamaduni wa kufanya kazi ambao unachochea ubunifu na mafunzo endelevu, na uboreshaji huduma. Kipaumbele kitatolewa kuendeleza usawa wa jinsia na kanda, hasa uwakilishi wa wanawake katika majukumu ya kiuongozi.

## Mawasiliano yenye tija ndani na nje

Mawasiliano ni njia ya ufunguo kwa ajili ya kuujenga ushirika na kwa ajili ya kulea mahusiano ya nje. Kwa njia ya mawasiliano mazuri tunataka kuelezea kisa chetu katika njia ambayo inahabarisha, elimisha, na inawavuta wahusika kutenda.

Tutaendelea kujihusisha kwa wakati, tukitengeneza sera na majukwaa yanayofaa kwa ajili ya kila mada na wahusika, kulingana na malengo yetu. Tutaendelea kukuza vyombo vya mawasiliano na njia zake. Tutahakikisha kuwa wale wanaohusika na mawasiliano wamepewa mafunzo ya kutosha na kazi yetu imewezeshwa kirasilimali vyakutoka.

*Mpango Mkakati huu uliandaliwa kwa njia ya mchakato wa pamoja, ambamo wengi walichangia. Tunatoa shukrani kwa wote walioshiriki katika kuandaliwa kwake: wajumbe wa Halmashauri Kuu na Kamati ya Utendaji ya FMKD, wawakilishi wa makanisa wanachama, mawakala tunaohusiana nao, washirika wa madhehebu mengine, na wafanyakazi wa ofisi ya fungamano.*

© Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, 2018

Imechapishwa na: Ofisi ya Mawasiliano
Idara ya mipango na utekelezaji

Anwani:
Route de Ferney 150
P. O. Box 2100
1211 Geneva 2, Switzerland

Tafsiri na Prof. Dkt. Faustin Leonard Mahali, Tumaini University Makumira, Tanzania

Sanifu: Weaver Creative
www.weavercreative.co.nz

ISBN: 978-2-940459-96-4

**Picha:**

Ukurasa wa mbele 1, 4, 7, 10, 24: FMKD/Albin Hillert
Ukurasa 16: FMKD/Brenda Platero
Ukurasa 21: FMKD/C. Kästner
Ukurasa 27: Therése Naomi Jonsson/Church of Sweden

FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI

*Tumekombolewa kwa neema ya Mungu, kuwa jumuiya ya Kikristo, tukiishi na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya ulimwengu wa haki, amani na uliopatanishwa.*

*FMKD Mpango Mkakati 2019-2024*

www.lutheranworld.org